

SIRI YA UONGOZI ILIYOFICHWA NDANI YA MICHEZO YA WATOTO "KULA TUMBAKISHIE BABA"

28 June, 2020



Niliwakuta watoto wanacheza, nikaona niwafafanulie falsafa hii.

"KULA TUMBAKISHIE BABA" ni mchezo wa watoto wenye umri kati ya miaka mitano (5) hadi kumi (10) ambao hawajatambua kama mchanga una vumbi linaloweza kuwachafua au kuwapa madhara.

UNAVYOCHEZWA; Unakusanywa mchanga kiasi (duara), kinachomekwa kijiti imara juu katikati ya duara. Wachezaji wanalizunguka duara hilo na kila mmoja atachukua mchanga kwa mkono mmoja kama wanavyokula chakula kwenye sinia, wakiwa wanaimba 'kula tumbakishie baba'. Mwishowe watakifikia kijiti, kwakuwa mchanga umeondolewa kitakosa egemeo na kudondoka. Mwelekeo wa kijiti ndio unaothibitisha kuwa aliyedondokewa ndiye aliyekula sana hivyo wachezaji wote watainuka na kumshambulia.

Lakini kabla ya mchezo kuanza kunawekwa mti au sehemu yakujiokoa, hiyo mkosaji anakimbia hadi kwenye mti huo na kushika. Ndipo ngumi, mateke na kuzomewa vinapokoma. Hairuhusiwi mtu yeyote kutoka nje ya wachezaji kuingilia mchezo hata kama anapenda au kutaka kutetea.

ELIMU; Tumekuwa mashuhuda hata kwenye mambo ya familia na mahusiano. Utalewa na rafiki zako, mtafanya uzinzi, watakutafutia michepuko lakini mke/mume akikukamata! Rafiki zako ndiyo watakuwa wakwanza

kukulaumu, kukucheka na kukutolea ushahidi wa uovu wako na picha watazitoa. Wala sio watu wa mbali nawe.

- 1. UONGOZI;** Kwenye uongozi kuchukua mchanga ni kutumia rasilimali za nchi lakini unatakiwa usilete madhara. Mfano uchimbaji wa madini, simamia uchimbaji wenye faida kwa jamii badala ya kuacha kuchimba ukiamini unatunza kwa vizazi vijavyo yakiwa aridhini.

Hivyo hivyo kwenye resources zingine. Kudondosha kijiti hapa ni kushindwa kusimamia na kusababisha matatizo kwa rasilimali hizo au kwa jamii ndiyo sababu wenzako wanaojua kuwa umezamisha boti, wanakushushia mkong'oto. Utashangaa Siku hizi kunaviongozi wakiwajibishwa wanalalama sana hadi kwenye mizimu ya babu zao watajua! Sijui hawakucheza mchezo huu?

- 2. KUKIMBIA NA KUJIOKOA;** Unafundisha unapohitaji kuwa kiongozi cha kwanza jitathmini kama unauwezo wakukabiliana na changamoto? Sababu kuna mahali utatakiwa kukimbia ili kuokoa au kujiokoa.
- 3. KUJIFUNZA KUKUBALIANA;** Mwendako anapokusanya mchanga mwingi nawe kidogo ni kwasababu ya woga wako au kiganja chako ni kidogo kuweza kuchukua

mchanga. Au umeibwa mchanga kipindi unaendelea kula, wanzako walikula mchanga uliokula. Mchanga ‘stands for people’.

Uhalisia: Iwe itikadi za kisiasa au dini, watu wako watakuwa wengi kutokana na njia unayotumia kuwapata na namna unavyowatunza na kuwawekea ulinzi. Badala ya matusi jikubali, boresha taratibu zako, ondoa woga, weka ulinzi wa hali au mali (wekeza)! Utapata wanachama wengi au waumini wengi kama ni dini.

4. **UNAFUNDISHA;** Unapokuwa kiongozi unaweza kuiba lakini usikamatwe. IBA USIKAMATWE! Hata ufisadi tunajifunza hapa hapa. Sasa wewe endelea kumpa mwanao PC na smartphone achezze game la nyoka na kujifunza kucheza pono za Kibrazil. Halafu unataka atoboe maisha kwakuwa fisadi.

Hongera washindi wa "KULA TUMBAKISHIE BABA" kwasababu mliuelewa vema mchezo huu. Na wale waliodondokewa na vijiti na wenzao wakawashushia vipigo! Hakuna kulalamika wala kulialia, kung'uta vumbi na simama. Kakae tena kwenye duara uendeleo kucheza utafanikiwa, tena zaidi kwakuwa kushindwa kulikuongezea maarifa. Ukisusa, Utakuwa umejiua mwenyewe.

Michezo hii ilitufundisha uvumilivu, kukabiliana na aibu, kutatua changamoto binafsi na jamii, kupitia mambo ya hatari ukitumaini mafanikio mbeleni. Waliocheza *karata za makwenzi*, wanaelewa ninachokielezea. Unapigwa, ukimaliza kulia unafuta machozi halafu unachanga karata na mchezo unaendelea.

Kombolela, watoto walijifunza kulinda mpira wakiwa wanafichua wachezaji kwa kutaja majina yao. Sasa wewe unapewa kitengo kimoja tu halafu watu wanakuja kubutua mpira mezani kwako kisha unanza kulalamika!